# Programu ya Nishati safi za Kupikia (CookFund): Kuharakisha upatikanaji wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia nchini Tanzania

## Mwongozo wa wito wa maandiko ya kuomba ufadhili

Final CFP (kiswahili)

### Muhtasari

Programu ya Nishati Safi za Kupikia (CookFund) , inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), ni mpango wa miaka mitatu (2022 - 2024) unaolenga kuharakisha upatikanaji wa nishati na vifaa bora vya kupikia Tanzania Bara, ukilenga mikoa mitano ambayo ni **Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza**. Mpango huo unatekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO). UNCDF ni Meneja wa Mfuko na mtekelezaji wa Mpango.

### Jedwali la maudhui

**1. Mandharinyuma**

**2. Kuhusu programu ya CookFund**

*2.1. Malengo*

*2.2. Walengwa wanufaika na maeneo*

*2.3. Teknolojia za kupikia lengwa*

*2.4. Biashara zinazostahiki*

*2.5. Utekelezaji wa washirika na wadau muhimu*

**3. Kuhusu wito wa maandiko ya kuomba ufadhili**

*3.1. Matumizi ya fedha*

*3.2. Aina ya msaada, kiasi na jamii za ufadhili*

*3.2.1. Kiasi cha fedha*

*3.2.2. Makundi ya fedha*

*3.3. Vigezo vya uteuzi*

*3.3.1. Mchakato wa uteuzi na Hatua muhimu za fedha*

*3.4. Mkataba*

*3.5. Mauzo na uhakiki*

*3.6. Mchakato wa ufuatiliaji na utoaji taarifa*

*3.7. Masoko ya mikopo ya kaboni*

**Viambatanishi**

*Kiambatanishi 1: Vigezo vya kustahiki*

*Kiambatanishi 2: Jedwali la tathmini*

*Kiambatanishi 3: Maelekezo ya kuwasilisha mapendekezo*

*Kiambatanishi 4: Warsha ya uwasilishaji wa awali kwa waombaji watarajiwa*

*Kutoridhishwa*

Final CFP (kiswahili)

# 1. Utangulizi

Ukosefu wa upatikanaji wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia ni changamoto ya kimataifa ambayo haiwezi kupuuzwa. Vikwazo vikuu vinavyozuia ukuaji wa sekta ya nishati safi ya kupikia ni tabia za watumiaji, uwezo wa kiuchumi, upatikanaji wa mikopo na (uelewa mdogo wa) uelewa tofauti na duni wa watumiaji. Juhudi za kitaifa za kuongeza matumizi ya nishati safi zinahitajika katika kusaidia upatikanaji wa nishati na vifaa pamoja na unafuu wa bei. Kutokana na uhitaji huu, shirika la UNCDF, kwa ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU), limeanzisha na kuzindua programu ya CookFund kwaajili ya kuharakisha upatikanaji wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia. Programu hii ilizinduliwa desemba 2021 na utekelezaji wake kwa mikoa yote mitano ni kwa miaka 3.

# 2. Kuhusu Programu ya Nishati safi za Kupikia (CookFund)

Programu ya Nishati safi za kupikia (CookFund) ni sehemu muhimu ya Mbinu Jumuishi ya Umoja wa Ulaya ya kuimarisha minyororo endelevu ya thamani ya nishati za kupikia nchini Tanzania na Mfuko wa 11 wa Maendeleo ya Ulaya (EDF), unaolenga kuchangia ahadi ya mabadiliko ya tabianchi ya Tanzania kwa kuongeza sehemu ya idadi ya watu wanaotumia nishati bora na endelevu za kupikia. CookFund ni programu inayotegemea utendaji ambayo itatoa msaada wa kifedha na kiufundi ili kusaidia kuharakisha upatikanaji wa nishati na vifaa bora vya kupikia (majiko na nishati) na hatimaye kuboresha mazingira, ajira, na fursa za biashara. Programu itatoa ruzuku ya msaada wa kitaalamu na kiufundi na ya ukuzaji wa mitaji ya uendeshaji na uwekezaji kwa makampuni yenye lengo kuu la kuongeza matumizi ya nishati safi na vifaa bora vya kupikia kwa mtumiaji wa mwisho na pia mtaji wa kufanya kazi na uwekezaji kwa biashara kwenye secta hii. Lengo ni kushughulikia changamoto za mitaji midogo, na hivyo kujenga uwezo wa biashara zinazohusika katika uzalishaji, uingizaji, usambazaji, jumla au rejareja wa majiko, nishati, au bidhaa na huduma zinazohusiana na kupika.

## 2.1. Malengo ya programu

Lengo kuu la mpango huu ni kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania kwa kuongeza idadi ya kaya zinazotumia nishati safi na vifaa bora vya kupikia. Lengo mahususi ni kuongeza matumizi ya njia za kisasa na safi za kupikia katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji kwa ajili ya kuboresha mazingira na ustawi shirikishi wa wananchi. Programu ya CookFund inakusudia kuziba pengo muhimu kati ya mitaji ya wawekezaji na mikopo.

## 2.2. Walengwa na wanufaika

CookFund inawalenga wasambazaji wa teknolojia na nishati safi za kupikia katika maeneo ya mijini katika mikoa lengwa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza. Wasambazaji walengwa ni pamoja na wazalishaji, waagizaji, wauzaji wa jumla, na mawakala wakuu wa teknolojia safi za kupikia. Lengo kuu la CookFund ni kuhamasisha biashara na wafanyabiashara kufikia kwa wakati na unafuu wa beiwatumiaji wa mwisho. Kipekee, uzalishaji wa majiko yenye ufanisi mkubwa wa matumizi ya nishati kwa huduma za kupikia kibiashara na ki-taasisi ili kuhudumia mahitaji muhimu utapewa uzingativu wa kipekee .

## 2.3. Teknolojia zinazolengwa

Mpango huu utatoa msaada wa kiufundi na kifedha kwa wafanyabiashara na mawakala wakuu wanaokidhi vigezo na kuhamasisha matumizi ya Gesi ya Petroli (LPG), Gesi Asilia iliyosafishwa (LNG), Bioethanol / Ethanol, majiko ya umeme, briquettes, na majiko ya mkaa yaliyoboreshwa (majiko ya mkaa yenye ufanisi wa nishati tu). CookFund inaweka msisitizo mkubwa juu ya utoaji wa huduma endelevu za kupikia zinazounganisha teknolojia safi za kupikia na nishati endelevu.

## 2.4. Biashara zinazokidhi Vigezo

Biashara na makampuni yanayokidhi kufadhiliwa na programu ya CookFund ni biashara ndogo na za kati (SMEs), makampuni

Final CFP (kiswahili)

na wavumbuzi wanaohusika katika teknolojia za kupikia zinazoendeshwa kibiashara na rafiki kwa mazingira. Ustahiki na kiwango cha fedha utazingatia biashara na waendeshaji, njia za kuwafikia watumiaji wa mwisho, uvumbuzi, ufanisi wa nishati na vifaa vya kupikia pamoja na upunguzaji wa hewa ya ukaa katika maeneo ya programu.

Makundi yafuatayo- ya biashara / makampuni yatazingatiwa:

- **Biashara ndogo na za kati (SMEs)** (wazalishaji, waagizaji, mawakala-wakuu wasambazaji, , wauzaji wa jumla, wauzaji wa rejareja) **wanaojihusisha na teknolojia mbalimbali safi za kupikia:** Hizi ni pamoja na makampuni ambayo yanaweza kuongeza uzalishaji na / au mauzo ili kupenya sokoni pamoja na yale yanayoweza kuagiza na kuiga teknolojia za kupika zilizothibitishwa.
- **Wabunifu wa njia za kidigitali za kulipia nishati za kupikia.** Hizi ni biashara zilizo na ufumbuzi na ubunifu kwenye vifaa na nishati za kupikia kwa watumiaji wa mwisho, hii ni kama vile mifumo rahisi ya malipo (kwa mfano, lipa kadiri ya matumizi), mbinu za kupata fedha ya mtaji, nk.

## 2.5. Washirika na wadau muhimu

Programu ya CookFund inasimamiwa na kutekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO). UNIDO inaelekeza ufadhili wake kwenye teknolojia ya kupikia ya bioethanol pekee katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**Mfuko wa Mitaji ya Maendeleo wa Umoja wa Mataifa** (UNCDF): UNCDF inafanya kazi kwenye sekta ya umma na binafsi kwenye nchi 46 duniani zenye kiwango duni cha maendeleo duni zaidi duniani. Likiwa shirika lenye mamlaka ya mitaji na zana za kifedha, UNCDF utao usaidizi wa kipekee ikilenga kufungua rasilimali za umma na za kibinafsi ili kusaidia kupunguza umaskini na kuinua maendeleo ya kiuchumi ya nchi husika. Kwa kuimarisha jinsi ambavyo fedha inaweza kufanya kazi na kuinua watu maskini katika kaya, biashara ndogo, na miundombinu ya kijamii, UNCDF inachangia malengo ya maendeleo endelevu ya kimataifa (SDGs) kwa kutambua sehemu hizo za soko ambapo ufadhili unaweza kuleta mabadiliko katika

CFP (kiswahili)

| DOKEZO MUHIMU |
|---|
| • Ufadhili utatolewa kwa njia mbili (i) **malipo kulingana na matokeo na (ii) malipo ya fedha za mitaji ya kufanyia kazi na mitaji ya uwekezaji** ili kuondoa changamoto za kimuundo katika soko, kujenga biashara na kuhamasisha kwa ufanisi aina mbalimbali za uwekezaji na kuwezesha upatikanaji wa mikopo. Ufadhili wowote utakaotolewa utafungamanishwa na idadi iliyothibitishwa ya watumiaji wa mwisho watakaofikiwa/kunufaika na mtoa huduma. Hivyo, makampuni / biashara zinazofadhiliwa zinapaswa kuzingatia takwa la ufadhili na kuweka taarifa za mauzo kwa watumiaji wa mwisho wanaofaidika na programu. |

kusaidia kufanikisha miradi mbalimbali na hivyo kupunguza matabaka kwenye jamii.

**Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO):** UNIDO ni shirika maalumu la Umoja wa Mataifa linalokuza maendeleo ya viwanda kwa ajili ya kupunguza umaskini, utandawazi jumuishi, na uendelevu wa mazingira. Dhamira ya UNIDO ni kukuza na kuharakisha maendeleo jumuishi na endelevu ya viwanda katika nchi wanachama. Vipaumbele vya kimkakati vya shirika ni pamoja na kujenga ustawi wa pamoja, kuendeleza ushindani wa kiuchumi, kulinda mazingira, kuimarisha maarifa na taasisi.

Washirika hao wawili wa utekelezaji (UNCDF na UNIDO) wanafanya kazi kwa kujenga ushirikiano imara na washirika wa ndani, kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa hizo ni pamoja na Wizara za Nishati (MoE), Maliasili na Utalii (MNRT), Fedha na Mipango (MoFP), Viwanda, Uwekezaji na Biashara (MIIT), Ofisi ya Makamu wa Rais (VPO) naOfisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Taasisi nyingine muhimu zitahusika kutokana na umuhimu wao ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Viwango Tanzania (TBS), Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Hewa Ukaa (NCMC), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA), na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF). Washirika wengine ni pamoja na Wawekezaji wa Kigeni (DFIs), taasisi nyingine za Umoja wa Mataifa, na sekta binafsi.

# 3. Kuhusu wito wa maandiko ya kuomba ufadhili

UNCDF inakaribisha wafanyabiashara wenye nia kutuma maombi ya kushindania ufadhili kwa njia ya maandishi kwenye awamu hii ya kwanza. Ufadhili utaendelea kutolewa kwa awamu tofauti kwa kipindi cha miaka mitatu chenye bajeti jumla ya EUR 9.7 milioni.

Kwa wito huu, UNCDF inakaribisha Biashara Ndogo na za Kati zinazokidhi vigezo (SMEs) na makampuni yanayoshiriki katika mnyororo wa thamani wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia na teknolojia zake katika Programu inayolenga maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji iliyotarajiwa kufikiwa. Msaada wa kifedha unalenga kutoa unafuu kwa watumiaji wa mwisho na pia kusaidia watoa huduma kuongeza mitaji kwa ajili ya kuwafikia watumiaji zaidi.

## 3.1. Matumizi ya fedha

Fedha zitatolewakwa matumizi mbalimbali kulingana na mahitaji ya biashara. Mwombaji atatakiwa kuainisha uhitaji wa fedha, na atahimizwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

- Kuboresha mkakati wa masoko na mauzo na ufanisi, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kukuza mbinu za masoko na mauzo.
- Kupanua biashara zinazohusiana na ufikishaji wa bidhaa na uwezeshaji wa malipo ya mtumiaji wa mwisho.
- Kuuza bidhaa mpya na / au kukuza ubunifu wa biashara kupitia uvumbuzi wa kidigitali kuongeza uwezo kwa watumiaji wa mwisho wa kupata bidhaa kwa urahisi na njia wezeshi za malipo yanayozingatia uwezo wao wa kipato.
- Mtaji wa kufanya kazi ili kupanua biashara na kuongeza uwezo wa kuwafikia watumiaji .
- Kuhamasisha watumiaji kwenye ngazi ya kaya kuhamia teknolojia safi ya kupikia yenye ufanisi wa nishati.
- Kutekeleza au kuimarisha mfumo wa taarifa muhimu za kimenejiment i ili kuboresha michakato ya biashara pamoja na vitengo vya kufuatilia na kutoa taarifa za mauzo.
- Kuongeza mitaji ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya uzalishaji, magari ya usambazaji, vifaa vya kuhifadhia vyote vikilenga kuongeza kiwango na ufanisi wa biashara, upatikanaji na usambazaji wa nishati.
- Waombaji wanaopendekeza matumizi mbadala ya ruzuku yasio miongoni mwa yaliyotajwa yatafikiriwa kwa njia za kipekee kutokana na umuhimu wake

## 3.2. Aina ya msaada, Viwango na Makundi ya ufadhili

Aina na kiwango cha msaada kitategemea mambo kadhaa kulingana na eneo la

Final CFP (kiswahili)

kijiografia, aina ya teknolojia, matumizi ya fedha (matumizi ya mtaji, mtaji wa kufanya kazi na / au ushauri wa kiufundi), uendelezaji wa masoko, maendeleo ya teknolojia, huduma bora/rafiki za malipo kwa mtumiaji wa mwisho, uboreshaji wa mnyororo wa usambazaji nk. *Angalia vigezo vya kukidhi kwenye kiambatanisho hapa chini.*

### 3.2.1. Kiasi cha fedha

Ufadhili utaanzia € 10,000 - € 300,000. Nyongeza ya Fedha yaweza kutolewa kutokana na utendaji wa mfadhiliwa na uwepo wa fedha kwenye mfuko.

Msaada wa kifedha kutoka kwa programu utakuwa kati ya asilimia 50% -75% ya jumla ya gharama ya mradi kwa biashara mpya au upanuzi unaohusishwa na msaada wa programu ya CookFund.
Kiasi cha fedha kinachotolewa kwa miradi kupitia CookFund kitaamuliwa baada ya uhakiki ikiwemo kutembelea mwombaji, na kufanya tathmini na upembuzi wa andiko la mradi na mpango wa biasahara.

### 3.2.2. Makundi ya Ufadhili

Fedha zitatolewa kwa ushindani ili kushughulikia vikwazo vya unafuu wa bei kwa mtumiaji wa mwisho pamoja na gharama kwa wafanyabiashara. Msaada mahsusipia utalengwa kupunguza gharama tangulizi za vifaa/teknolojia. Ufadhili unaosemwa utatolewa kupitia makundimatatu yaliyoangaziwa hapa chini:

**Kundi la Kwanza:** Inahusisha ufadhili kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara pamoja na ruzuku inayotolewa kulingana na matokeo ya kiwango cha mauzo kilichowafikia watumiaji wa mwisho kikiwa na unafuu wa bei. Ruzuku itatolewa kulingana na idadi ya mauzo kwa watumiaji wa mwisho na ni baada ya ukaguzi na uthibitisho.

Ufadhili katika kundi hili unatofautiana kulingana na aina ya nishati husika. Pia inatofautiana kulingana na ukubwa wa kifaa au teknolojia husika (mf. Mtungi wa gesi wa 6kg Vs 15kg)

Kwa ruzuku inayolewa kulingana na matokeo ya mauzo kwa wateja wa mwisho, watalazimika kwanza kuuza kiasi cha majiko walichoahidi baadaye kuomba kupatiwa ruzuku.

Aina ya teknolojia iliyokubaliwa yaani, jiko la shinikizo la umeme (EPC), jiko umeme la kupikia wali, Jiko la mkaa lililoboreshwa (ICS), Jiko la bioethanol, n.k. ni lazima yatimize vigezo vya ubora vinavyokubalika ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa na shirika la viwango na ubora Tanzania.

Ili kuhamasisha biashara na makampuni yanayokidhi vigezo , zoezi la uhakiki litafanyika katika mzunguko wa kila baada ya miezi mitatu au baada ya kuuza idadi inayoahidiwa mara nne kwa mwaka. (*Angalia vigezo vya kustahiki na kuchagulika hapa chini*.) Kutakuwepo na mawasilano kabla ya mabadiliko yoyote ya viwango vya ruzuku/motisha.

*Jedwali no.1. linaonyesha viwango vya ufadhili kwa kila makundi tofauti ya huduma.*

~~**Kundi la Pili:**. Kiwango cha mtaji wa ukuzaji na uendeshaji wa biashara utapimwa kwa idadi ya majiko yaliyouzwa y kwa watumiaji wa mwisho. Ruzuku ya fedha itatolewa kwa hatua~~

Final CFP (kiswahili)

*Table 1. CookFund awards/Incentive Levels per Technology*

| Category | Cooking Solution | Initial Investment Grant | Performance based subsidy | Total of subsidy (advanced pre-financing + RBF) | Target | Explanatory Note |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.1 | Electric Cookers for Households | € 16 equivalent to TZS 38,000 per projected unit to be imported | € 13 equivalent to TZS 30,000 per unit sold to end users | € 29 equivalent to TZS 68,000 per unit | Proposed units to be imported and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application. | Detailed proof of importation should be provided to support the initial grant. |
| 1.2 | Bioethanol | € 14 equivalent to TZS 33,000 per projected unit to be imported | € 9 equivalent to TZS 20,000 per unit sold to end users | € 23 equivalent to TZS 53,000 per unit | Proposed units to be imported and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Support for Bioethanol exclude Dar es salaam region which is covered under UNIDO support. |
| 1.3.1 | LNG/LPG (6Kg Cylinder) with single burner | € 2.0 equivalent to TZS 4,500 per projected new unit to be purchased | € 2.2 equivalent to TZS 5,500 per unit sold to new customers | € 4.2 equivalent to TZS 10,000 per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | "New unit" means a new cylinder not used.<br><br>"New customer" means that, the end user is buying the bottle for the first time.<br><br>Applicants to cat 1.3 can propose in their application multiple |

Final CFP (kiswahili)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | sub-categories (1.3.1 to 1.3.6, etc) |
| 1.3.2 | LNG/LPG (15Kg Cylinder) | € 3.0 equivalent to TZS 7,700 per projected new unit to be purchased | € 4.0 equivalent to TZS 9,600 per unit sold to new customers | € 7 equivalent to TZS 17,300 per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Same as 1.3.1 |
| 1.3.3 | LNG/LPG (38 Kg Cylinder) | € 5.0 equivalent to TZS 12,900 per projected new unit to be purchased | € 7.0 equivalent to TZS 15,900 per unit sold to new customers | € 12 equivalent to TZS 28,800 per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Same as 1.3.1 |
| 1.3.4 | LNG/LPG (3 Kg Cylinder) | € 1.3 equivalent to TZS 3,100 per projected new unit to be purchased | € 1.7 equivalent to TZS 4,000 per unit sold to new customers | € 3.0 equivalent to TZS 7,100 per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Same as 1.3.1 |
| 1.3.5 | LNG/LPG (10 Kg Cylinder) | € 3.5 equivalent to TZS 8,000 per projected new unit to be purchased | € 4.2 equivalent to TZS 10,240 per unit sold to new customers | € 7.7 equivalent to TZS 18,240 per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | This is specific for cylinders integrated with PAYGO systems. |

Final CFP (kiswahili)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.3.6 | LPG Stoves (double or more burners)[1] | 14% of the verified retail market price per projected new unit to be sold | 18% of the verified retail market price per projected new unit to be sold | Total 32% of the retail market price per unit | Proposed units to be purchased and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Imported stoves should meet standards set by TBS. If produced locally, the stoves must pass TBS certification (efficiency & durability) |
| 4 | ICS | € 1.6 equivalent to TZS 3,800 per projected unit to be produced | € 2 equivalent to TZS 4,700 per unit sold to new customers | € 3.6 equivalent to TZS 8,500 per unit | Proposed units to be produced and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | The stove must be certified by TBS to have passed the efficiency and durability tests. |
| 5 | Briquettes | € 0.18 equivalent to TZS 430 per projected unit (kg) to be produced | € 0.22 equivalent to TZS 530 per unit sold to new customers | € 0.4 equivalent to TZS 960 per unit | Proposed units to be produced and sold in order to benefit from the cook fund must be detailed in the application | Business sustainability and markets should be clearly demonstrated by applicants. |

Final CFP (kiswahili)

[1] *LPG stoves will only be considered when offered as a package along LPG gas cylinders by super dealers.*

**Kundi la Pili Mtaji wa uwekezaji na kuendesha biashara –"PAYGO":**. Programu hii ya CookFund inahamasisha ubunifu wa kidigitali katika kuwafikishia huduma watumiaji wa mwisho. Ufadhili wa mtaji wa kuwekeza na wa kuendesha biashara utatolea wa waombaji wenye kutua huduma hii kama vile utoaji wa mbinu rafiki za kurahisisha malipo ya bidhaa na huduma.

Kwa waombaji wa kundi hili, programu itatoa ufadhili wa 60% kufadhili shughuli kma vile uagizaji wa vifaa/teknolojia kutoka nje. Kwa waagizaji watapokea ufadhili mara baada ya kutoa nyaraka za uthibitisho wa uagizaji huo. Salio la 40% litatolewa baada ya uthibitisho wa kufikisha huduma kwa mlaji/mtumiaji wa mwisho.

**Kumbuka:** *CookFund haifidii au kurejesha gharama ambazo tayari zimeshawekezwa, kwa mfano, majiko yaliyopelekwa hapo awali au uwekezaji uliofanyika kabla.*

## 3.3. Vigezo vya Kuchaguliwa

Unafuu wa bei ya huduma/bidhaa kwa mtumiaji wa mwisho ni kigezo cha msingi na lazima kichanganuliwe kwa takwimu na mwombaji na kuthibitishwa na UNCDF, (*angalia mwongozo wa ujazaji wa fomu uliyotolewa kama kiambatanisho cha mfano*).

Waombaji watatathminiwa kulingana na vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na malengo na viwango vya mauzo, uzoefu wa biashara na soko la nishati, ufanisi wa nishati husika, uzalishaji mdogo wa hewa ya ukaa; upatikanaji wa bidhaa zinapohitajika, ubunifu kwenye uuzaji na kuwafikia walengwa/wateja na kiwango cha mchango kufikia malengo ya mradi na maendeleo endelevu na kiwango na kasi ya ukuaji wa biashara. Sifa za kuchagulika pia zitazingatia usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi na masuala ya kijamii na mazingira.

***Muhimu:*** *Uhalisia wa mipango ya ukuaji wa biashara ya mwombaji utazingatiwa zaidi kuliko mipango ambao ni ya kunadharia zaidi.*

### 3.3.1. Mchakato wa uteuzi na Hatua muhimu za fedha

Ili kuhakikisha kuwepo kwa mipango mizuri ya kibiashara, ya kuaminika na kuwawezesha waombaji kushiriki bila kuwekeza rasilimali kubwa katika hatua ya awali, mchakato wa maombi utafanyika kwa awamu tatu kama ilivyoelekezwa hapa chini.

i. **Upembuzi wa kwanza (Toka orodha ndefu ya waombaji):** Hii itafanywa na timu ya usimamizi wa mfuko (Meneja wa Mfuko na maafisa uwekezaji) mara baada ya kupokea maombi. Meneja wa Mfuko ataangalia namna ambayo maombi yamewasilishwa kukidhi vigezo muhimu vilivyoainishwa kwenye fomu ya maombi

ii. **Upembuzi wa pili (Toka orodha ya waliofanikiwa kupita vigezo kwenye upembuzi wa kwanza):** Meneja wa Mfuko na maafisa uwekezaji watazingatia tathmini ya sifa za mradi zifuatazo:

   a. Uchambuzi wa kina wa mahitaji ya mtaji wa kazi na uwekezaji katika mradi, na kiwango cha mtaji wa mwekezaji/mfanyabiashara husika.
   b. Uchambuzi wa kina wa sifa za mradi: mtaji wa kutosheleza; Kiwango cha uwekezaji wa vifaa nya kuzalishia, aina ya teknologia,umri wa biashara na uuzaji wa technologia ya kupikia iliyothibitishwa; ina maisha marefu ya kiutendaji na kiuchumi; ina pato la kiuchumi ambalo linaamuliwa hasa na muundo wake wenye mafanikio.
   c. Uendelevu wa kiuchumi na kifedha wa kibiashara au kampuni.
   d. Athari au matokeo chanya ya teknologia inayotumika au kuuza
   e. Matokeo yanayopimika na yanayoonekana hasa ya kijamii, kiuchumi ikiwepo idadi/kiwango cha mauzo, ajira zitakazozalishwa, uwezo wa kuwafikia walengwa au watumiaji na unafuu wa bei.
   f. Matokeo ya Ziada ya ya mradi: Ruzuku haikusudii kupotosha, kubadilisha au kuwa mbadala ya huduma au msaada mwingine au kuondoa nia ya kupata mikopo ya kibiashara.

Final CFP (kiswahili)

g. Kumbukumbu za kuthibitisha rekodi za nyuma za utendaji
*h.* Bei pendekezwa za nishati safi za kupikia ukilinganisha na za kipindi hiki cha uombaji.

**Zingatia***:* Maombi ya ufadhili yataorodheshwa na kufadhiliwa kulingana na jinsi maombi na biashara ya mwombaji ilivvyokidhi vigezo stahiki vya Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia "CooKfund".

iii. **Tathmini ya Mradi/Biashara ya Mwombaji:** Hatua hii inafuatia kwa wale waliofanikiwa katika mchujo wa hatua ya kwanza na ya pili. Tathmini hii itafanywa na Meneja wa Mfuko na maofisa wawekezaji na itahusisha:

a. Tathmini ya kina ikiwa ni pamoja na kutembelea eneo husika la biashara;
b. Tathmini na uthibitisho wa ukweli wa taarifa zilizowasilishwa kwenye andiko la mradi na hali halisi ya ya taarifa zilizopo kwenye nyaraka za ofisi za mwombaji;
c. Utengnezaji wa muhtasari wa taarifa zilizopatikana kwa hatua nyingine muhimu zitakazofuata;

Wakati wa hatua ya mwisho ya tathmini, waombaji waliofanikiwa watahitajika kukamilisha na kusaini makubaliano ya utekelezaji kabla ya makataba wa utoaji wa ruzuku.

## 3.4. Mkataba na Makubaliano

Waombaji watakaofanikiwa wataingia mkataba au makuliano ya kimaandishi juu ya kiwango na matarajio yao ya mauzo wakati wa kipindi cha mkataba.

## 3.5. Mauzo na uhakiki

Makampuni na biashara zitakazopata ufadhili zinapaswa kuthibitisha bei za sasa wanazolipa watumiaji wao wa rejareja na zile watakazo watoza baada ya kupata ufadhili. Kutakuwa na mpango maalumu wa jinsi ya kuthibitisha na kuweka kumbukumbu ya mauzo ya ziadi yaliyofanywa na watakao pata ufadhili.

## 3.6. Mchakato wa ufuatiliaji na utoaji taarifa

- Waombaji wanaofanikiwa watapaswa kuwa tayari kutoa maelezo ya kina wakati wote wa muda wa mkataba, ikiwa ni pamoja na taarifa za mauzo na matokeo chanya kwa maendeleo ya taifa.
- Waombaji wanaofanikiwa watafikiriwa kupata msaada wa ziada wa kiufundi katika kuanzisha mifumo muhimu ya teknologia ya habari na mawasiliano (tehama) kwa ajili ya kutolea taarifa za programu.

## 3.7. Masoko ya Hewa ya Ukaa

Kwa hiari na utashi wao wenyewe wafanyabiashara au makampuni yanayouza nishati safi ya kupikia wanaweza kufungamanisha matokeo ya kazi zao na programu za kitaifa (National Carbon Monitoring Centre) za kupata mapato yatokanayo na mauzo ya hewa ya ukaa. Umoja wa Ulaya na UNCDF hazitadai au kufaidika na mapato yatokanayo na biashara hii ya hewa ya ukaa. Ikiwezekana faida iende kwa watumiaji wa mwisho wa nishati safi ya kupikia katika maeneo husika.

Final CFP (kiswahili)

# Viambatanishi

## Kiambatanishi 1: Vigezo vya kustahiki ufadhili

Programu ya Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) iko wazi kwa biashara na makampuni ambayo yatakuwa na vigezo vifuatavyo:

i. *Wigo wa Kijiografia:* Kuwa na shughuli katika maeneo ya mijini ya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza pekee. ***KUMBUKA: Walengwa katika nishati ya kupikia ya bio-ethanol kwa Dar es Salaam tu wanapaswa kuomba kupitia dirisha tofauti ambalo linasimamiwa na UNIDO (v.akim@unido.org).***

ii. *Upeo wa Kimaumbile na* Ustahiki wa Bidhaa: Imelenga kuzingatia teknolojia na nishati safi za kupikia (LPG, Gesi Asilia, Ethanol, Umeme, Briquettes, na ICS) na viwango vya ubora vinavyohusiana na taratibu za ubora zilizoainishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

iii. Ukubwa na aina ya mahitaji ya fedha uwiane na viwango vya bajeti zinazotolewa katika kwenye wito huu.

iv. *Kwa biashara zinazozalisha faida na makampuni yanayolenga soko:* Kuwa tayari na biashara inayoendelea, mpango wa biashara ulioelezewa vizuri, mtiririko chanya wa fedha na faida, au kuonyesha njia wazi ya upanuzi na faida kufuatia msaada wa Programu hii.

v. Mahitaji ya uwezo wa kitaalamu;
   - Waombaji wanapaswa kuonyesha kuwa wana rasilimali za kutosha, uwezo na uzoefu kuhimili kufanya biashara katika soko la nishati safi ya kupikia.
   - Waombaji pia watahitajika kuwa na timu muhimu ya menejiment na uongozi watakaohusika na usimamizi na utekelezaji na uratibu wa biashara/mradi uliofadhiliwa
   - Wafanyakazi wanapaswa kuwa na sifa stahiki za utekelezaji wa shughuli za mradi zilizopendekezwa.

vi. Uzoefu na Ujuzi wa soko;
   - Waombaji wanapaswa kuonyesha kuwa wana uzoefu wa kutosha wa biashara na soko la nishati safi ya kupikia katika maeneo husika ya programu hii.

vii. Fedha zinazoombwa hazipaswi kuwa mbadala wa fedha zilizokwisha tengwa au kuidhinishwa awali kwa matumizi ya kitaifa katika sekta/sekta ndogo husika au mbadala wa mikopo ya kibiashara inayopatikana kwa watoa huduma ya mikopo . Hii ni kwa mujibu wa kanuni za EU kuhusiana na ongezeko (additionality)

viii. Mwombaji aliyefanikiwa kukidhi vigezo vya kupokea fedha za Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) anapaswa kufungua akaunti tofauti ya benki ya kupokea na kutolea au kulipa fedha kwenye vifungu vilivyoainishwa na kukubalika. Ruzuku hii ya fedha anayopewa mfanyabiashara au kampuni haipaswi kutumika kuhudumia majukumu ya kifedha yaliyokuwepo awali kama madeni ya biashara, mikopo ya binafsi au ya-kibenki n.k

ix. *Matokeo tarajiwa na mfumo wa biashara unaohusisha kuuza kwa watumiiaji wa ngazi za kaya au biashara ndogo ndogo au taasisi. Ili kupokea ufadhili waombaji waliofaulu vigezo* wanatakiwa kutoa na kuuza huduma za nishati safi za kupikia, zenye ubora uliothibitishwa na kwa bei inayohimilika moja kwa moja kwa watumiaji wa mwisho kwa njia endelevu.

x. Ufuatiliaji na Utoaji wa Taarifa: Uwezo wa mwombaji na utayari wa kufuatilia na kutoa taarifa za mauzo kwa watumiaji wa mwisho wa teknolojia, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa data na ukaguzi wa ubora wa data. Takwimu za msingi juu ya utendaji uliopo zinapaswa kutolewa.

Final CFP (kiswahili)

xi. *Uthibitisho wa takwimu na nyaraka za shughuli za biashara husika na uzoefu:* Kuwa na angalau mwaka mmoja wa shughuli za biashara na rekodi za chini za kifedha au uthibitisho kuwa taarifa za kifedha za biashara ndani ya miezi sita (6) baada ya utoaji wa ruzuku.

xii. *Utii wa sheria na Taratibu:* Mwombaji awe mzingatiaji wa sheria za nchi (Tanzania), na za kimataifa, kanuni na taratibu zilizopo zikiwemo za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Viwango vya Utendaji wa Mazingira na Jamii na kanuni za haki za binadamu hasa katika mazingira mazuri ya kazi.

xiii. *Uhalali na hali ya Sasa ya biashara:* Iliyoanzishwa, na kusajiliwa kisheria na inafanya kazi nchini Tanzania kwa mujibu wa sheria.

xiv. Mazingira na uendelevu: Kwa waombaji wa biashara za bioethanol na mkaa mbadala wa peleti (briquettes) wanapaswa kuonyesha kwamba nishati yoyote inayostahiki kutumiwa inazalishwa au kupatikana kwa njia endelevu, ikiwa ni pamoja na utengenezaji endelevu wa mkaa mbadala au peleti. Uthibitisho unapaswa kutolewa wakati wa hatua ya maombi juu ya vyanzo vya malighafi zinazotumika na athari zake kwa mazingira, yaani, ukataji miti au aina nyingine ya uharibifu wa kiikolojia.

xv. Uimarishaji wa haki za kijinsia.

- Waombaji wanahimizwa kutoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake kupitia sera zao wenyewe na taratibu za ajira ikiwa in pamoja na miradi inayopendekezwa.
- Hii itatathminiwa kupimwa na hali ya sasa ya menejimenti, oungozi na uendeshaji wa sasa wa biashara ya mwombaji (upendeleo maalum utatolewa kwa makampuni yenye uwakilishi wa usawa wa kijinsia katika ngazi zote za kihierakia na usawa wa malipo ).
- Waombaji wanaofanikiwa watahitajika kuendeleza mipango ya utekelezaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na mkakati wa masoko / uhamasishaji ambao ni sikivu kwa mahitaji na motisha za wanawake na wanaume kwa kununua nishati safi za kupikia.

Final CFP (Swahili)

## Kiambatanishi 2: Jedwali la tathmini

| Vigezo | Ufafanuzi | Pointi | Alama ya jumla |
|---|---|---|---|
| **Yasiyo ya kifedha** | Upembuzi wa jumla wa kiufundi na ki-teknologia wanishati safi ya kupikia | 10 | 60 |
| | Kufanya biashara ya nishati safi ya kupikia ndani ya wigo wa kijiografia wa mikoa mitano husika | 5 | |
| | Mpango wa biashara ulioandaliwa vizuri:<br>• Muhtasari wa wazi na wakilishi wa maeneo/mambo muhimu na wezeshi ya kufanikisha malengo ya biashara<br>• Maelezo mahsusi yahusuyo kampuni na/au biashara na bidhaa zinazouzwa<br>• Mipango na mikakati ya mauzo na masoko | 25 | |
| | Uwezo wa kufuatilia na kutolea taarifa za mauzo ya mtumiaji wa mwisho wa nishati husika | 5 | |
| | Uwezo wa kampuni/biashara na wa timu ya menejimenti (ikiwa ni pamoja na tathmini ya uzoefu, ujuzi na uwezo wa kufuatilia) na ki-uutawala wa mwombaji. Pia tahmini ya rekodi ya kufuatilia shughuli zingine, kiwango cha muda wa utendaji na ukomavu kibiashara | 10 | |
| | Mazingatio na uhuishwaji wa kijinsia katika biashara | 5 | |
| **Ya kifedha** | Mchango na matokeo ya bei wezeshi inayomlenga mnunuzi au mtumiaji wa mwisho wa nishati safi ya kupikia | 25 | 40 |
| | Utendaji wa kifedha wa vipindi vilivyopita na makadirio na makisio ya utendaji wa kifedha ikiwa biashara au kampuni itapata ufadhili toka kwenye programu. | 10 | |
| | Uwepo na upatikanaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa miaka ya hivi karibuni ya uendeshaji wa biashara. | 5 | |

Final CFP (kiswahili)

## Kiambatanishi 3: Maelekezo ya kuwasilisha mapendekezo

Mawasilisho yote yanapaswa kufanywa kwa kuijaza kwa ukamilifu fomu maalum ya maombi itakayokupakuliwa kutoka anwani hii hapa: *https://uncdf.link/CfP-CookFund-Tanzania-SW*

Fomu ya maombi **lazima iwasilishwe** katika muundo wake wa awali (Microsoft Word) pamoja na nyaraka zozote zinazohusika kwa anwani ya barua pepe ifuatayo: cookfund.tz@uncdf.org Kichwa cha somo cha barua pepe ya wasilisho lako kinapaswa kuwa na maneno **CookFund_JINA LA MWOMBAJI**. Kwa mfano, ikiwa jina la biashara au kampuni yako ni **ABC Limited**, kichwa cha somo cha barua pepe yako kitakuwa "CookFund_ABC Limited". Ukubwa wa barua pepe unapaswa kutokuzidi MB 10.

***Lugha ya pendekezo na sarafu: Andiko na*** Mapendekezo ya biashara yanapaswa kuwasilishwa kwa lugha ya Kiingereza. Taarifa za kifedha zinapaswa kuwasilishwa kwa kutumia TZS au Euro. *Endapo kutatokea mkanganyiko wa tafsiri, tangazo la lugha ya kiingereza linachukuliwa kuwa tangazo la msingi.*

***Muda na Tarehe ya mwisho ya Uwasilishaji: Maombi ya*** awamu ya kwanza andiko la ufadhili wa mradi wa CookFund yatafunguliwa mnamo **1 Septemba 2022** na kubaki wazi hadi **16 Disemba 2022**. Tathmini na mapitio ya maombi itafanywa kwa kila ombi lililowasilishwa hadi mwisho wa awamu ya kwanza. Duru za ziada za maombi mengine zitatangazwa kwa vipindi tofauti ndani ya miaka 3 ya utekelezaji wa programu ya nishati safi ya kupikia.

***Jambo Muhimu la Kuzingatia:*** Mara baada ya kuwasilishwa, maombi yatachukuliwa kuwa ya mwisho na hayawezi kurekebishwa kabla ya mapitio na upembuzi wa awali na maoni ya UNCDF. Waombaji wasiokidhi vigezo kwa awamu ya kwanza watapata fursa ya kuelekezwa na kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili waweze kuwasilisha maombi yaliyorekebishwa

Kwa habari zaidi na / au maswali, tafadhali wasiliana na:
UNCDF Tanzania, barua pepe: *cookfund.tz@uncdf.org*
Tel: +255 22 260 0911

## Kiambatanishi 4: Warsha ya uwasilishaji wa awamu ya kwanza kwa waombaji watarajiwa

UNCDF inapanga kuwakaribisha wafanyabiashara walengwa kwenye warsha za nusu siku ili kuwaongoza na kuelekeza waombaji juu ya mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa na kuwasilisha maombi ya ufadhili. Lengo la warsha hizi ambazo zitafanyika katika miji ya Mwanza, Dodoma, Morogoro, Kibaha na Dar es Salaam kwa nyakati tofauti ni kuwapa waombaji fursa ya kuibua maswali na kutaka ufafanuzi toka UNCDF ili kuongeza uelewa ili maombi yaweze kukidhi vigezo vya kustahiki na uteuzi.

Kushiriki au kutokushriki ni hiari na wala sio kigezo cha kupata au kutokupata ufadhili. Ikiwa unataka kushiriki, tafadhali tuma barua pepe kwa *cookfund.tz@uncdf.org* inayoonyesha *" warsha kabla ya uwasilishaji wa wito kwa UNCDF"* katika kichwa cha somo la barua pepe yako. Tafadhali pia onyesha ni mkoa upi ambao utapenda kushiriki kati ya mikoa mitano iliyolengwa yaani, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Dodoma na Mwanza. Muda na ukumbi wa warsha utajulishwa kwa wakati unaofaa kwa wale ambao wataomba ushiriki. Waombaji watatakiwa kujilipia gharama zao zote za kuhudhuria warsha hii. Gharama za ukumbi na mafunzo zitalipwa na waandazi wa warsha.

Final CFP (kiswahili)

## Maombi ya Taarifa Za Ziada

Ili kutenda haki na kufanya maamuzi sahihi kwa waombaji, UNCDF itakuwa na haki ya kuomba maelezo ya ziada kutoka kwa waombaji katika hatua yoyote ya mchakato wa maombi. UNCDF ina haki ya kurekebisha na / au kuongeza zaidi vigezo vya kustahiki na mahitaji ya chini, pamoja na mwongozo mwingine wowote unaohusiana na CookFund, uliotolewa hapa au mahali pengine. Ikiwa kutakuwa na mabadiliko, Waombaji watajulishwa kwa wakati unaofaa kabla ya kumalizika kwa muda wa mwisho wa maombi kwa awamu hii ya kwanza.

Final CFP (kiswahili)